

**KIS 220: ORAL LITERATURE IN KISWAHILI**  
**MAIN EXAM**

**STREAM: BED (Arts)****Time: 3 hours****MAAGIZO KWA WANAFUNZI**

- (i) *Jibu swalii la KWANZA na maswali mengine MAWILI*
- (ii) *Usiandike katika karatasi ya mtihani*

**Swali la Kwanza**

(a) Fafanua dhana zifuatazo kama zinavyotumiwa katika fasihi simulizi. (Alama 10)

- i. Sanaa
- ii. Maghani
- iii. Fanani
- iv. Muundo
- v. Mandhari

(b) Ukizingatia hoja NNE, bainisha umuhimu wa nadharia za fasihi simulizi. (Alama 8)

(c) Fafanua hatua kuu TATU za kuhakiki kazi za fasihi simulizi. (Alama 12)

**Swali la Pili**

Jadili uainishaji wa fasihi simulizi chini ya vigezo vifuatavyo. (Alama 20)

- i. Muundo
- ii. Maudhui au yaliyomo
- iii. Wahusika
- iv. Namna ya uwasilishaji
- v. Lugha inayotumika

**Swali la Tatu**

Mabadiliko ya kisiasa, kiuchumi, kijamii, kiutamaduni, kidini, kielimu, kiteknolojia na hata katika usafiri husababisha tanzu mbalimbali za fasihi simulizi kubadilika (Masebo na Nyangwine, 2016). Uhirejelea kauli hii, dhihirisha athari HASI za usasa katika angalau sekta TANO zilizotajwa na wataalamu hawa. (Alama 20)

**Swali la Nne**

- (a) Fasili mshabaha uliopo kati ya fasihi simulizi na andishi kwa hoja TANO. (Alama 10)
- (b) Fasihi simulizi ina sifa zinazoihalalisha kuwa sanaa. Zipambanue sifa TANO. (Alama 10)

**Swali la Tano**

Umesoma maoni katika gazeti moja kuwa fasihi simulizi haina nafasi yoyote katika fasihi andishi. Kama mkereketwa wa fasihi simulizi, pambanua hoja TANO ambazo utazizingatia katika kupinga maoni hayo. (Alama 20)

\*\*\*\*\*